Hii Yaweza Kuwa Siku Ya Mwisho Ya Uhai Wako?

na

Ellis Forsman

Hii Yaweza Kuwa Siku Ya Mwisho Ya Uhai Wako?

na

Ellis Forsman

Oktoba 11, 2011

Hii Yawezakuwa Siku Ya Mwisho Ya Uhai Wako?

Luka 12:13-34

Watu wengi wanaogopa kifo.

Je umewahi kufikiria kuhusu kufa? Umewahi kufikiria kutokuwa na wapendwa wako ambao utawaacha nyuma? Unafikiria itakuwiaje wewe baada ya kufa? Unafikiria biashara ambayo haijakamilika hapa kabla hujafa? Unafikiria, “Bwana, siko tayari kwenda bado!”?

Ndg. Otto Alvarez alikuja Lorenzo muda fulani huko nyuma na kuongea na sisi kuhusu kazi aliyokuwa anafanya Mexico, na zaidi alivyo ongea na kujibu maswali ya watu yaliyomlenga, ndivyo alivyopata furaha. Kwa hatua fulani alisema, “Nina uhakika Bwana anakuja usiku huu!” Ndugu mmoja akasema kwamba alijifikiria mwenyewe kwa wakati huo, “Waah! Siko tayari kwa hilo, bado!

Wakati mtu anatoa wazo kwamba maisha haya yanaweza kufika tamati, kuna kuwa na hali ambayo si salama ambayo wengi wetu wanaanza kuhisi. Hatuko pekee yetu katika hisia hizo; hakika mara nyingi kunakuwa na uoga unaohusika katika kujadili somo hili.

Wakati watu wanapokumbwa na swala la kifo uamzi wao juu ya swala hili lina kuwa kubwa, ikitegemea kwamba ni Wakristo ama si Wakristo. Mtu wa dunia, mara nyingi kama sio zote, angeweza kuchagua kutokufikiria kifo kamwe.

Yohana Wayne, akiwa na miaka 71, alieleza kwamba wakati mwingine anakuwa na ugumu anapoangalia picha zake za zamani. Alisema, “Ni kama inatisha nikiona nilivyokuwa na mtazamo mzuri nikiwa na miaka 40, na ghafla naweza kuona na kutazama miaka hii 71…Si lalamiki, nawakumbusha… nataka niwepo kwa muda mrefu.”

Woody Allen wakati fulani alisema, “Siyo kwamba naogopa kifo. Sitaki tu kuwepo pale inapotokea.”

Leo, baadhi ya uoga wa watu dhidi ya kifo una nguvu na ujasiri wao katika teknolojia ni mkuu kiasi kwamba wanatumia makumi ya madola ili kuwezesha miili yao ikaushwe wakati wanapo kufa. Tumaini yao ni kwamba waweze kupokewa na kuishi tena tiba inapopatikana kwa cho chote kitakacho sababisha kifo chao.

Watu wengi wanakuwa na hofu nyingi ya mawazo kwamba maisha yao yanafikia tamati. Louis wa XV, mfalme wa Ufaransa, aliogopa kifo kiasi kwamba aliamuru neno "kifo" isitamkwe kamwe katika uwepo wake. Pia aliagiza kwamba kila sanamu iondolewe katika sehemu ambayo hataweza kuona sura ya mtu ambaye tayari amesha kufa, ili kwamba asije akakumbushwa kwamba yeye, binafsi, wakati fulani atakufa. Lakini kwa uoga wake wote, Louis wa XV alikufa kwa ugonjwa wa pepo punda Mei 10, 1774.

Watu wengi wanaweza kutambua kwa hisia za wafalme wa Ufaransa. Kwa upande mwingine, tunaona sayansi ya kipekee na uhitimisho ya madawa kwa miongo michache. Imekuwa ikisemwa kwamba mtu wa kawaida katika mji wake leo anaweza kutibu ugonjwa vizuri kuliko madaktari miaka sabini na tano iliyopita. Lakini kwa upande mwingine, tunaanza kuhisi kwamba sayansi na teknolojia haitaweza kuturuhusu kuishi milele katika maisha haya.

Watu wengi wanadhani kifo kwao ni mwendo mrefu.

Bila kujali yanayoweza kutokea wakati ujao, bado kuna wazo katika akili za watu wengi kwamba watakuwa hai kwa miaka mingi ijayo.

Hawawezi kujileta wenyewe na kufikiria uwezekano kwamba uhai wao utafika tamati kwa siku zijazo. Kwa nini hili? Labda ni kwa sababu watu wanabanwa sana na shughuli zingine. Wanabanwa na kutengeneza pesa, kununua mashamba, kujenga majumba, kulea watoto, na kwa ujumla kujaribu kulipa madeni. Wanabanwa sana, hakika, kwamba wanasahau kuomba na kujifunza Biblia na kwenda kanisani na kuishi maisha ya uungu. Watu wengi wanaotuzunguka leo wapo bila dira maalum, bila kusudi lo lote, na bila mfumo wo wote wa maisha yanayo kubalika zaidi mbele za uso wa Mungu.

Kama hawawezi kupunguza kasi na kukaa chini na kufikiria kuhusu swala hili, basi wanapaswa kukiri kwamba wakati unakuja ambapo wote tutakufa. Ujuzi wa mwanadamu unatuambia kwamba hili ndivyo, na mara nyingi tunapita kipimo, imesisitizwa zaidi. Watu wanaweza kwenda msibani na kusikia mhubiri anasoma maneno ya Ayubu kutoka katika Biblia:

Ayubu 14:1-2, "*Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu. Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa, hukimbia kama kivuli wala hakai kamwe.*"

Mkristo wa kweli anatazama kifo kama mlango wa kupitia kwenda katika uzima ulio mkuu ambayo Mungu anayo katika hazina yake kwa

waaminifu. Wale Wakristo wanaokaa nyuma pasipo kulia kwa sababu ya Wakristo wenzao wamekufa na wamekwenda milele, na kwa sababu ya wapendwa watakumbukwa hadi watakapokutana tena.

Lazaro alipokuwa amekufa kwa siku nne Yesu aliwakuta Mariamu na Martha wakilia kwa sababu ya kumpoteza Lazaro. Yesu mwenyewe pia alilia kwa sababu ya huruma yake dhidi ya wanawake hawa waliokuwa na huzuni nyingi, hata ivyo alifahamu (Yesu) kwamba Lazaro alikuwa pamoja na Mungu. Yesu alitumia nafasi hii kama muda wa kuonyesha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu kwa kumfufua Lazaro kutoka katika wafu, ili kwamba wengine waweze kuamini.

Watu wengine kwa kuwapoteza wanafamilia waliowapenda wanalia kwa siku kadhaa, majuma, miezi, na hata wakati mwingine miaka. Kiafya haimpasi mtu kuruhusu akili yake ifikirie kwa muda mrefu kwa kuwapoteza wapendwa wao.

Watu wanafahamu yote haya, sasa ni kwa nini bado wanaendelea na pirika za maisha haya bila kutengeneza mipangilio kwa ajili ya maisha yajayo? Labda katika shughuli zao zote, wameweka imani yao nyingi katika neno “kesho”. Ndiyo, wanaweza kupoteza kazi zao – kesho. Wanaweza kuugua – kesho. Wanaweza kufa – kesho. Lakini, kulingana na mambo ya leo, hayo ni mambo tu yanayowatokea watu wengine.

Inaweza kutufanyia vyema kupunguza kasi ya maisha na kufikria kuhusu swali: Hii yaweza kuwa siku ya mwisho ya maisha yangu? Saa ya kioo inamkimbia kila mmoja. Yawezekana ikakukimbia hata wewe leo? Kunaweza kukawa na mchanga uliosalia katika saa yako ya kioo? Yaweza kuwa hii ndiyo siku ya mwisho ya uhai wako?

Hatuwezi kuepuka kufa

Hatuwezi kuishi milele.

Ukweli ni kwamba hatutaishi milele katika maisha haya. Kulikuwa na mtu katika Biblia aliyesahau ukweli huo, na Bwana akatoa mfano juu yake; tunaiita mfano wa tajiri mpumbavu. Ilikuwa ni hadithi ya mtu aliyemiliki shamba kubwa. Mungu akaangaza jua na kunyeshea mvua, na shamba hili lilikuwa na musimu wenye mafanikio. Hakika, wakati wa mavuno alikuwa na mavuno ambayo ghala lake lisingeweza kubeba, hivyo akaamua kuharibu maghala yake na kujenga makubwa. Baada ya yote, alikuwa na pesa nyingi katika hazina na ulinzi mwingi kwa ajili ya baadaye.

Luka 12:17-19, "*Akaanza kuwaza moyoni mwake akisema nifanyeje? Maana sina pa kuyaweka akiba mavuno yangu. Akasema nitafanya hivi; nitazivunja ghala zangu nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kisha, nitajiambia, Ee nafsi yangu una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi.*"

Lakini Yesu alimwita mtu huyo mpumbavu:

Luka 12:20-21, "*Lakini Mungu akamwambia mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nini? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.*"

Mtu huyu alisahau kwamba kifo ni hakika na kwamba ni ghafla, ukweli halisi wa maisha. Pia alisahau kwamba Mungu anayetoa uzima ana uwezo wa kuuchukua tena. Sasa huyu mkulima mwenye mafanikio hakuishi kufurahia mafanikio haya. Hatupaswi kuwa wajinga kiasi hicho!

Wengi wanaficha uoga wao dhidi ya kifo "mafanikio".

Leo hii watu wanaweza kuficha uoga wa kufa vizuri. Wanaweza kuufunika kwa dhana ya "mafanikio" yao. Wanaweza kujiambia, "Nitauonyesha ulimwengu uthamani wangu – nitapata pesa. Nitanunua kila kitu ninachokiitaji. Nitakwenda katika sherehe zote. Nitainuka wa kwanza katika kampuni na mfalme wa milima, na hakuna mtu atakayenizuia."

Lakini watu wanapaswa kusikiliza maneno ya wale ambao tayari wameshafikia mafanikio katika uso wa ulimwengu. Wengi wao husema hawana furaha na maisha yao.

Hebu tusiamini uongo wa shetani kwamba kifo hakitatugusa miaka mingi ijayo. Anataka tusahau uasilia wa maisha unaopita, na anajaribu kutushawishi kwamba furaha huja kutokana na kutengeneza pesa nyingi, kwenda katika sherehe nyingi, na kujaribu kupitia matukio yaliyojiri. Kwa bahati mbaya, hatuambii kwamba vitu hivi vyote vitakwisha kwa wakati, na kwamba tunapaswa kumwona Mungu katika Hukumu.

Kuna watu ambao wana mafanikio katika uso wa ulimwengu, lakini siku moja watakufa na kuzikwa katika majeneza mazuri ikipambwa na maua mazuri. Alafu Kristo atawaambia, "Ninyi wapumbavu."

Kifo kinatuijia sisi sote, na ikiwezekana haraka tofauti na tunavyo dhani.

Hata mtu anapoishi maisha ya kawaida, wakati unapita haraka. Kama Ayubu alivyosema: Ayu. 7:6, "*Siku zangu hupita upesi kuliko chombo cha kufumia, nazo zapita pasipokuwa na matumaini.*"

Umewahi kuona ua la zamani? Ule mchipuo wa kati unavyouzunguka ua, na kila tukio linachukua dakika. Kauli iliyozoeleka tunayoisikia kwa wazee ni, "Maisha yanaendaje haraka nini kimetokea kwa miaka yote?" Mara nyingi wataongelea vitu vilivyotokea nusu karne iliyopita kana kwamba yalitokea jana. Hebu wote tuakikishe kwamba tunaelewa kwamba hatuwezi kuzuia wakati – pia hatuwezi kuipunguza kasi. Hakika itakwenda haraka kuliko "roketi"

Maisha yanaweza kukoma ghafla

Hadithi ya tajiri mpumbavu pia inapaswa kutufundisha kwamba maisha yaweza kufikia ukomo ghafla. Mungu alisema, Luka 12:20, "*…mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako…*"

Tajiri mpumbavu alikuwa mkulima mwenye mafanikio na pia alikuwa mfanya biashara mzuri. Hakuna uthibitisho kwamba hakuwa mtiifu au raia mbaya katika jamii. Hakutambua tu kwamba ni haraka kiasi gani uzima wake ungeondolewa. Angeweza kushindilia jembe la ng'ombe ardhini, lakini asingeweza kuondoa kaburi usiku huo. Hakupanga kukutana na Mungu kati ya masaa machache yajayo.

Watu wengi wanadhani kwamba watakuwa tayari kwa kifo. Wanafikiria kwamba watawaita wanafamilia waizunguke kitanda na kusoma mirathi na kusema kwaheri kwa kila mmoja, lakini haikutokea kwa njia hiyo. Watu wengi wanakufa pasipo kutarajia. Hakuna onyo kwamba inakwenda kuwa siku yao ya mwisho ya uhai wao.

Wakati mwingine, unasoma matangazo ya vifo kwenye magazeti. Kuna maswala machache ambapo wanafamilia wajua kwamba kifo kilikua kinakuja haraka. Hakuna mtu aliye na uwezo wa kuzuia hili linapotokea wakati maisha yake yatakapofikia tamati labda ajinyonge. Ni juu ya Bwana wakati muda wetu ukifika.

Yakobo 4:13-15, "*Haya basi ninyi msemao leo au kesho tutaingia katika mji fulani na kukaa humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida; walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni*

nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha kutoweka. Badala ya kusema, Bwana akipenda tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi."

Watu wengi zaidi hawafanyiki Wakristo hadi wapate kila kitu ambacho ni kamilifu katika maisha yao. Lakini Yesu anasema uzima ni bure. Iko kwa muda mfupi alafu hutoweka. Ndege huanguka, magari ugongana, nyumba zinaungua, magonjwa yanaua, na pumzi ya uzima unatoweka.

Tutaishije sasa?

Haitishi, lakini kutii. Hatupaswi kutishika kwa wazo la kifo. Paulo alikuwa na tabia njema dhidi ya kifo.

1 Kor. 15:55-57, "*Ku wapi ewe mauti, kushinda kwako? U wapi ewe mauti uchungu wako? Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Jibu la uoga wa kifo ni kutii injili na kuishi maisha ambayo ni ya uaminifu kwa injili hiyo. Kutii injili inamaanisha kujinyenyekeza sisi wenyewe kwa mapenzi ya Mungu na kutii maagizo yake. Kufanyika Mkristo, lazima tu:

Amini. Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanaye pekee ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Tubu. Luka 13:3, "*Nawaambieni sivyo, lakini msipotubu mtaangamia vivyo hivyo.*"

Mkiri Kristo. Mat. 10:32-33, "*Atakayenikiri mbele ya watu nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali atakayenikana mbele za watu nami nitamkana mbele za Baba yangu aliyembinguni.*"

Ubatizwe. Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Mara tunapotii injili, mara baraka za Mungu huja juu yetu.

Mtume Paulo alisema: 2 Kor. 5:1-8, "*Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni. Maana katika nyumba hii twaugua, tukitamani sana kuvikwa*

kao letu litokalo mbinguni; ikiwa tukiisha kuvikwa hatutaonekana tu uchi. Kwa sababu sisi tulio katika maskani hii twaugua tukilemewa si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa, ili kitu kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima. Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya neno lilo hilo ni Mungu aliyetupa arabuni ya Roho. Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. Maana twaenenda kwa imani si kwa kuona. Lakini tuna moyo mkuu nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana."

Wengine husema wanataka kuifikiria kwa muda kabla hawajafanyika Wakristo. Tatizo la "lifikirie kwanza" ni kwamba hakutakuwa na muda mwingi wa fikra hiyo.

Kila mtu lazima afanye uamuzi

Injili ya Kristo inamlazimisha kila mmoja wetu kufanya uamzi leo. Mtu hafanyiki Mkristo kwa bahati mbaya au kwa kosa kwa sababu aliishi katika familia ya Kikristo. Mtu hajikwai kwa kufanyika Mkristo. Ni maamzi ya dhamira ndiyo tanapaswa yafanyike. Na uamzi huo haupaswi kuchukua siku, wiki, miezi au miaka ili uweze kuufanya. Mifano inayofungamana katika maandiko ya Agano Jipya ambapo maamzi ya kufanyika Mkristo ulifanyika hapo kwa hapo.

Mdo. 2:38-41, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"

Filipo na Towashi. Mdo. 8:26-39, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo akamwambia ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, Towashi mwenye mamlaka chini ya kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena je*

yamekuelea haya unayoyasoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwanakondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule Towashi akamjibu Filipo, akisema, nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji, yule towashi akasema, tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu aksema naamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame wakatelemka wote wawili majini Filipo na yule Towashi naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule Towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria."

Watu wengi wanaposhikwa na usingizi usiku huu, watakuwa wanafikiria mambo mengi. Hali ya hewa itakuwaje kesho? Teni gani linapaswa kulipwa kesho? Kazi itakwendaje kesho? Kesho nitafanyaje michezo? Je kijana huyo mzuri ataniomba tutoke leo?

Lakini swali halisi linapaswa kuwa: Kama Bwana akiniita nitoke katika maish haya usiku huu, je nitakuwa tayari kukutana naye kwenye hukumu? Tajiri mpumbavu alifanya kosa baya kwa kuweka imani yake katika uwezo wake binafsi wa kuishi na kujilinda mwenyewe, badala ya kuishi kwa utii kwa Mungu na kuweka imani yake kwake.

Ama tukiondoka katika maisha haya usiku huu au hapana, ukweli ni kwamba miaka mia kwanzia sasa, wote tulioko leo tutakuwa tumeshakufa. Hatima yetu itakuwa imeshafunikwa – ama umilele mbinguni, au motoni. Chaguo lako liko mikononi mwako.

Lazima tuanze kupanga leo kwa ajili ya uzima wa milele tuliopewa. Je uko tayari kuanza leo katika hiyo bara bara inayoongoza kwenda mbinguni?